# Uhusika wa Mwanamke katika Nyimbo za Kizazi Kipya Tanzania

Steven E. Mrikaria

**Ikisiri**

*Uhusika wa Mwanamke ni dhana iliyojadiliwa kwa mapana kupitia nyimbo za Kiswahili za muziki wa dansi, taarabu, dini na hata nyimbo za kizazi kipya kila wakati. Katika makala yetu, tumeonesha namna uhusika wa mwanamke ulivyosawiriwa katika nyimbo za kizazi kipya kwa kupitia maneno ya nyimbo za wasanii Ben Pol, Mwasiti Ft. Linnah, Zainab Lipangile, Barnaba Boy, Twenty Percent, Dayna Feat Marlaw, Vick Kamata, Nakaya Sumari, Diamond Platmamz, Lady Jay Dee, Jaguar Kenya, Ally Kiba na Banana Zoro. Katika uchambuzi wetu, tumeyanukuu baadhi ya maneno ya nyimbo hizo kwa lengo la kushadidia kile kinachozungumzwa juu ya uhusika wa mwanamke katika jamii inayomzunguka.*

*Tumetumia nadharia ya ufeministi, hususani ufeministi wa Kiafrika, katika kuyajadili matatizo anayokabiliana nayo mwanamke wa Kitanzania hususani katika kipengele cha udhalilishwaji, ukandamizwaji na udunishwaji wake. Aidha, makala yetu imeujadili uhusika wa mwanamke dhidi ya tabaka kandamizi katika jamii kwa kuijadili dhana ya mwanamke huyu na uhusika wake katika nyimbo za kizazi kipya. Makala imezipitia na kuzichambua nyimbo za Kiswahili za kizazi kipya. Mwishoni tumehitimisha na kupendekeza nini kifanyike ili kumkwamua mwanamke huyu.*

## 1.0 Utangulizi

Masuala ya uhusika wa mwanamke katika fasihi ya Kiswahili yamejadiliwa na waandishi wanawake na wanaume kwa kipindi kirefu bila ya kufikia makubaliano ya namna ya kuendeleza mapambano ya mwanamke dhidi ya tabaka kandamizi. Mapambano haya yameendelezwa na Mwachofi, (1987) na Mazrui, (1982) ambao walisimama kidete wakizishambulia kaida na tamaduni zinazochangia katika kumkandamiza mwanamke kwani ndizo zinazousukuma ukandamizwaji wao. Wasomi hawa wameuzungumzia uhusika wa mwanamke kwa kuwatetea na kuwapigania pale wanaponyimwa haki zao. Morris, (1993) amewajadili Mwachofi na Mazrui (khj), akisema kuwa, tofauti kati ya uhusika wa mwanamke na mwanamume husababishwa na mgawanyo holela wa majukumu yao uliotokana na maumbile yao ya kibiolojia. Anasema kuwa, wanawake wanabaguliwa kwa kuonekana dhaifu na kwa mujibu wa utaratibu wa kimaisha na kijamii uhusika wao unajitokeza tokea utotoni kwa sababu ya tamaduni za Kiafrika.

Momanyi, (2000) amehitimisha kuwa, mwanamke amehusishwa na chombo cha kumstarehesha, kumpamba, kumpendezesha, kumvutia na kumlea mwanamume na

familia nzima kwa ujumla. Masuala ya uhusika wa mwanamke kutokuangaliwa kwa macho ya usawa akilinganishwa na mwanamume yamechambuliwa na yataendelea kuchambuliwa hadi wanawake watakapojikomboa. Kujikomboa kwao kunatakiwa kuanzie katika nyanja za kitamaduni, kisiasa, kiuchumi na kifikra. Kwa kupitia nyimbo za kizazi kipya ndipo mwanamke atakapoweza kupambana na kujikwamua kutokana na changamoto zinazoukabili uhusika wake katika jamii inayomzunguka. Katika kuchunguza maudhui ya nyimbo za wasanii tajwa hapo juu, tunatarajia kutafuta suluhisho na kutoa mapendekezo yanayotokana na maswali yafuatayo:

a) Ni kwa kiasi gani waimbaji na wasanii wa nyimbo hizo wanaweza kuubadilisha uhusika wa mwanamke uliozoeleka kwa kupitia maneno na utendaji wao katika jamii inayowazunguka?
b) Ni kwa namna gani wasanii wa kike na wa kiume wa nyimbo hizo wanavyoweza kuzibadilisha kaida za kiutamaduni na kijamii zinazohusiana na uhusika wa mwanamke na mwanamume?
c) Nyimbo za kizazi kipya zinahusikaje katika kushawishi uwiano wa kiutendaji baina ya wanawake na wanaume katika jamii ya Kitanzania?

Katika kutafuta majibu ya maswali yetu hayo, ni lazima kuchunguza kwa kina uhusika wa mwanamke na jinsi unavyochorwa katika baadhi ya nyimbo za wasanii wa kizazi kipya, kwa kuangalia namna uhusika wake ulivyochorwa.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Makala hii itaongozwa na nadharia ya Ufeministi, ambayo inaangalia uhusiano kati ya mwanamume na mwanamke. Kwa mujibu wa Khonje, (1979) na Mackinnon, (1991) nadharia ya Ufeministi ilianza mwanzoni mwa miaka ya 1792 huko Ulaya, katika nchi za Uingereza na Marekani. Katika kipindi hicho wanawake hawakuthaminiwa katika jamii zao, ambapo walikuwa ni watu wa daraja la chini. Aidha, wanawake hawakuhusishwa katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile kuwachagua viongozi kwa kupiga kura au kuchaguliwa katika uongozi. Sehemu iliyoonekana kuwafaa wanawake ilikuwa nyumbani, hususani katika shughuli za jikoni, kulea watoto na kumhudumia mwanamume.

Mackinnon, (1991) anadai kwamba, ufeministi ni nadharia ya kwanza iliyoibuliwa na kundi la watu waliovutiwa na mustakabali wake na wa maendeleo ya wanawake duniani kote. Anazitaja sababu tatu muhimu za wataalamu kujishughulisha na kuyajadili masuala ya wanamke kuwa ni: Kwanza, wanawake wamekuwapo katika kundi la wanaotawaliwa na wanaume kwa muda mrefu mno bila ya kukombolewa. Pili, wanawake wamefanywa kuwa wategemezi katika jamii, sio kwa sababu ya asili ya mtu au ya kibiolojia, bali ni kutokana na mfumo dume unaozizunguka jamii zetu. Na tatu, ni kutokana na mgawanyo usio sawia wa majukumu, unaomkandamiza

mwanamke kuwa katika kiwango cha chini cha kazi zisizo na hadhi katika jamii na kumwona mwanamke kama chombo na si binadamu kama mwanamume.

Baada ya wanawake kuona kwamba wamewekwa katika daraja la mwisho kwenye ngazi zote za maamuzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, ndipo walipoamua kuanzisha harakati za kujikomboa wenyewe (Wamitila, 2002). Hapo ndipo yalipoanza mapambano yaliyopigwa vita katika miaka ya 1800 mpaka 1900 ambapo, madai yao kama kudai haki ya kupiga kura, kupata nafasi katika ngazi za kiuchumi na kijamii yalianza kukubalika.

Nadharia ya ufeministi inatoa fursa ya kuchunguza na kubaini jinsi asasi za kijamii zinavyoshirikiana kutatua na kuimarisha tofauti za kijinsia katika kumsawiri mwanamke katika fasihi. Ni kwa kupitia nadharia ya ufeministi ndipo tutakapoweza kuyabainisha maovu wanayofanyiwa wanawake katika maeneo kadha wa kadha ya kiukandamizwaji na ya kiudhalilishwaji duniani. Makala haya yamejadili na kuchambua dhana ya uhusika na utendaji wa mwanamke kwa kupitia maneno ya nyimbo za wasanii kumi na tatu wa kizazi kipya na kutoa maoni na mapendekezo yetu.

**3.0 Dhana ya Mwanamke katika Nyimbo za Kizazi Kipya**

Wafula na wenzake, (2007) wanatueleza kuwa, masuala ya wanawake yalianza kushughuliwa karne ya 19 na kufikia upeo wake miaka ya 60 na 70 ya karne ya ishirini. Wanaeleza kuwa, katika karne ya ishirini ndipo wanawake wa Magharibi walipoanza kuzungumzia masuala yao haya katika maandishi. Sote tumeishuhudia nadharia ya ufeministi inavyoendesha mapambano ya kumkomboa mwanamke kutoka katika mfumo kandamizi wa kiutamaduni unaoendeshwa duniani kote hadi leo hii. Pamoja na jitihada tunazoziona zikiendelea, bado unyanyaswaji na unyimwaji wa haki kwa wanawake katika nyanja nyingi na kuu za maisha umezidi kushamiri na kuongezeka.

Kwa mujibu wa mtandao wa jinsia (TGNP 2001), katika Bara la Afrika hususani Kusini mwa jangwa la Sahara, wanawake wamewekwa katika kundi la wanyonge na walioachwa nyuma kiasi cha kutokufaidi hali ya usawa wakilinganishwa na wanaume katika kupewa huduma za kijamii. Mbilinyi na wenzake, (1991) wameyaona haya nchini Tanzania na kusema kuwa, wanawake wanaonewa kuanzia nyumbani hadi katika jamii nzima ya leo. Lyatuu, (2011); ameyaona waliyoyasema Mbilinyi na wenzake na akapendekeza kwamba, elimu ndiyo mkombozi wa mwanamke wa kumwezesha kujitoa katika mfumo kandamizi wa wanaume. Lyatuu anasisitiza kwamba, elimu itasamsaidia mwanamke kuondokana na mawazo potofu ya wafeministi wa Kiafrika wanaodai kwamba nafasi hiyo waliyopewa wanawake ni kwa mapenzi ya Mungu. Mawazo na fikra yakinifu za wapambanaji wa uhusika wa mwanamke wa Kiafrika kama Mwachofi, (1987); Mazrui, (1982); Mbilinyi na

wenzake, (1991); Morris, (1993); Momanyi, (2000); TGNP, (2001); Wafula na wenzake, (2007); ( Lyatuu, (2011) na wanaharakati wengine wengi hayatuzuii kujadili uhusika wa mwanamke katika nyimbo za kizazi kipya nchini Tanzania.

Uhusika wa mwanamke umekuwa ukipitia nyanja mbalimbali za udhalilishwaji, unyanyaswaji na ukwezwaji kutokana na majukumu na utendaji wake wa kazi aliogawiwa na jamii yake. Mgawanyo huo wa majukumu umewasaidia wasanii wakifeministi kumchambua na kumsawiri mwanamke kama kiumbe jasiri, mvumilivu shujaa na mwenye kustahili kusifiwa kutokana na uwezo wake wa kuzalisha mali na kuiendeleza jamii yake. Makala yetu itatumia mawazo haya chanya ya wasanii wa kifeministi na kisha kuuchambua uhusika wa mwanamke kupitia taswira kadhaa zinazooneshwa na wasanii wasiokuwa wafeministi wa nyimbo za kizazi kipya Tanzania. Baadhi ya taswira zitakazochambuliwa ni mwanamke kama *chombo cha starehe*, mwanamke kama *kiumbe tegemezi*, mwanamke kama *malaya* na mwanamke kama *mtu mwenye wivu*, tutakazozichambua na kuzijadili katika sehemu ya nne ya makala yetu.

Kwa mfano, zipo baadhi ya nyimbo za kizazi kipya zilizomsawiri mwanamke kama kiumbe ya mpole, mvumilivu na mwenye utu wema, tunauona uhusika wake ukiambatana na tabia njema, busara, uaminifu, heshima, upendo na uzazi mwema. Baadhi ya nyimbo hizo ni ule wa msanii Ben Pol, *Nitakupata* ambapo msanii huyu ametuchorea jinsi uhusika wa mwanamke unavyothaminishwa na mambo aliyowahi kuyafanya maishani mwake. Msanii anawachora marafiki aliokuwa nao, warembo alioshirikiana si kwa sababu tu ya kuwa na mali nyingi bali kwa sababu ya tabia, wema na ukarimu. Msanii katika wimbo wake huo anasikika akisema:

(1) ...*Uzuri sio sura ma, Pozi na maumbile kama wengine wanavyodhani*
*Bali uzuri ni tabia, Hekima na ukarimu wako. Busara na Imani*
*Na nikikupata milele nitafurahi, Nitaimba nakupenda,*
*Nitaimba nakupenda hadi mwisho wa uhai...*

Katika kifungu hiki cha wimbo *Nikikupata,* msanii Ben Pol ameonesha umuhimu wa tabia nzuri, hekima, busara na mzuri katika kumudu kukaa na mwanamume. Msanii anasisitiza kuwa, uhusika wa mwanamke haujadiliwi kwa kuiangalia sura, maumbile na mwonekano wa nje wa mwanamke bali hujitokeza katika matendo na mwenendo wake kwa jamii.

Wapo wasanii wa nyimbo za kizazi kipya waliomchora mwanamke kama mtu mwenye msimamo usioyumba na awezaye kutoa maamuzi ya kipekee kabisa. Wasanii hawa wamesisitiza kuwa, endapo mwanamke atakataa au atataka kufanya jambo lake fulani la kimapenzi, kiitikadi, kimaendeleo na hata la kimalezi, atalifanya kwa kila hali ilimradi afanikishe azma yake. Wasanii kwa mfano, Mwasiti

amemwonesha mwanamke kama mtu anayeweza kuamua jambo lolote ambalo anataka lifanyike na likafanyika bila kipingamizi. Tunaposikiliza wimbo wake *Nalivua Pendo* msanii anasema:

(2) ... *Leo nalivua pendo, nililopenda zamani.*
*Nabadili wangu mwendo, ili niwe furahani*

Katika kipande hiki kifupi, tunamwona mwanamke akiwa amechoshwa na utegemezi kwa mwanamume na kuamua kujitoa katika penzi, alilolianza na alilokuwa akiliendeleza kwa muda mrefu. Kujitoa huko ndiko alikokuangalia Mackinnon, (1991) katika nadharia ya ufeministi na kusema kwamba, haiwezekani wanawake wakawa tegemezi kwa wanaume kwa kuunga mkono mfumo dume unaozizunguka jamii nyingi. Tunaoneshwa kuwa, uhusika wa mwanamke katika kuwa na mapenzi ya dhati, ulichezewa kwa kuvurugwa na mwanamume aliyekuwa na tabia mbaya. Wimbo huu unamwonesha mwanamke akiwa amekerwa na manyanyaso ya mwanamume na hivyo, kuamua kujitoa kwenye penzi ili aweze kufurahia maisha. Mwasiti katika wimbo wake huo anaonesha msimamo thabiti wa mwanamke katika kufanya maamuzi unaohusu maisha yake na ya jamii inayomzunguka. Tunaoneshwa jinsi msichana Rina alivyokuwa mwenye furaha, mapenzi, vicheko na starehe mara baada ya kuolewa kutokana na kupendwa na kutumikiwa na mume wake. Mwisho wa starehe hizo alizokuwa akipewa ulifika baada ya miaka kupita ambapo, mume wake alibadilika kiasi cha kumchefua Rina hadi kutoa uamuzi mzito wa kuachana na mume wake wa ndoa. Mifano tuliyoiona hapo juu kupitia kwa wasanii Ben Pol na Mwasiti inatuonesha kuwa, kuna haja ya kuwaangalia, kuwachunguza na kuwachambua wasanii wengine wa nyimbo za kizazi kipya nchini Tanzania ili kufahamu jinsi walivyousawiri uhusika wa mwanamke katika nyimbo zao.

Kwa upande mwingine, Omari, (2009) alipokuwa akichambua maudhui ya muziki wa kizazi kipya anatuambia kwamba, ili wimbo uweze kufikisha ujumbe vizuri kwa hadhira, na kuweza kukubalika kwa wapenzi wake, msanii hana budi kubuni msamiati na maneno yanayowakilisha dhana mbalimbali za kuwavutia wasikilizaji wake. Hii ndio sababu iliyowasukuma baadhi ya wasanii wa kizazi kipya kutumia ufundi wao wa kimsamiati kumsawiri mwanamke katika miktadha mbalimbali inayomkandamiza kama vile; kiumbe tegemezi, laghai, malaya, msaliti na kadhalika. Aidha, wapo wasanii wanaomtazama mwanamke wakimkweza pale alipostahili kukweza na wakimsifia pale alipostahili kusifiwa. Wasanii hawa wamemsawiri mwanamke kama nguzo ya familia, mtu wa kuheshimiwa, mtu wa kutetea na mtu wa kupiganiwa pale wanapomwona akidhalilishwa na kunyimwa haki zake. Mitizamo hii na mingine mingi tutaijadili na kuichambua huku tukizipitia baadhi ya nyimbo za wasanii wa nyimbo za kizazi kipya.

## 4.0 Uhusika wa Mwanamke katika Nyimbo za Kizazi Kipya

Uhusika wa mwanamke katika nyimbo za kizazi kipya tutakazozipitia unajitokeza kwa njia zifuatazo:

- kama kiumbe dhaifu na duni,
- kama chombo cha starehe na mfanyabiashara ya ngono,
- mwanamke kunyimwa fursa ya kupata elimu na kujishughulisha na siasa,
- kama mtegemezi kwa mwanamume, na
- kama mzazi, mlezi na mwenye huruma.

Katika makala yetu hatutaweza kuyajadili yote hayo, bali tutayapitia na kuyachambua machache kama ifuatavyo:

### 4.1 Mwanamke kama Kiumbe Dhaifu na Duni

Kumwita mwanamke kiumbe dhaifu na duni ni kumdharau na kumdunisha kuwa hana, hawezi na hafahamu lolote. Huu ni unyanyaswaji ulioanzishwa hapo zamani, wakati mwanamke aliponyimwa sauti juu ya mwanamume katika mfumo mzima wa maisha. Kwa mujibu wa nadharia ya ufeministi, unyanyasaji, ukandamizaji na udhalilishaji wa mwanamke, uliendeleza ubabe dume, hadi karne ya 19, ambapo wanaharakati wa nadharia hii waliamua kumtetea mwanamke huyu. Katika miaka ya karibuni, wanawake kwa kupitia wanaharakati wa kifeministi na wale wa haki za binadamu waliikataa dhana ya kuwa wao ni dhaifu na hivyo kujitosa katika kufanya kazi mbalimbali zinazohitaji nguvu na mamlaka. Ndio maana tunawaona wanawake wakifanya kazi katika mitambo ya umeme, kufanya kazi za nyumbani na kushika nyadhifa kubwa serikalini. Juhudi hizi za wanawake kuhusishwa na kufanya kazi kwa ufanisi zimeonwa na msanii wa nyimbo za Zainab Lipangile katika wimbo wake wa *Mama Afrika*. Msanii huyu anasikika akisema:

(3) *... Mimi mama Afrika, Sauti yangu nasikiika, Afrika x 4*
*Mama Afrika, Nafasi nashika, Machoni pa watu, Nakubalika,*
*natetea wanawake wa Kiafrika, Kimawazo kamwe sitafilisika,*
*watoto wa kike wanabakwa kwa ajili ya pipi pipi na ofa,...*

*... Mimi mama Afrika, Sauti yangu nasikiika, Afrika x 4*
*Tumeumbika ulimwengu mzima tunakubalika,*
*Tunasikitishwa na wasichana wa Kiafrika,*
*Siku zinavyozidi wanazidi kuharibika,*
*Sitosita kuwaelimisha ...*

Msanii amemchora na kumwonesha mwanamke shujaa wa Kiafrika, *Mama wa Afrika* anayeshikilia nafasi ya juu kabisa ya kuwatetea wanawake wengine wa Kiafrika duniani. Tunamwona msanii akiwataka wanawake kuwajibika ili waweze

kujikomboa na kuondokana na kuwategemea wanaume. Msanii anawahamasisha wanawake kuepukana na madhila ya wanaume kwani wengi wao ni wadanganyifu.

Zipo tamaduni anazokulia mwanamke, zinazochangia katika kumdidimiza mwanamke na hivyo, kuidumaza nafsi yake na mwishowe ikamsuta kuwa yeye ni kiumbe duni. Tamaduni kama hizi wameziona watafiti wa fasihi kama vile Lughano, (1989) na Ndung'o, (1999) ambao katika kazi zao wamezishambulia tamaduni hizi zinazomdunisha mwanamke kama ilivyo kwenye utamaduni wa baadhi ya wanajamii wa Kiafrika. Matokeo ya tafiti zao yameonesha kuwa, mwanamke ameonewa, amedunishwa na kuwekwa katika nafasi ya pili baada ya mwanamume kutokana na tamaduni za jamii husika. Makala imekwenda mbali zaidi kwa kuishauri nadharia ya ufeministi kujipanga vema katika kuuangalia utamaduni wa mwanamke anayelazimishwa au kulazimika kupokea vitu vya thamani alivyonunuliwa na mwanamume vinavyompelekea kumbakwa na kudhalilishwa na mwanamume huyu. Ni kwa kupitia msimamo na maamuzi ya wananadharia hii ndipo tunapoweza kuurekebisha utamaduni huo unapotosha utu wa mwanamke wa Kitanzania. Tafakari nzuri tunaipata katika wimbo wa Zainab Lipangile *Mama Afrika* akisema:

(3b) *... Kimawazo kamwe sitafilisika,*
*watoto wa kike wanabakwa*
*kwa ajili ya pipi pipi na ofa,...*

Mawazo na tamaduni hizi zimewalemaza baadhi ya wanawake na wanaume ambao hadi hivi leo wanaamini kwamba mtoaji mkuu wa fedha au zawadi ni mwanaume.

### 4.2 Mwanamke kama Chombo cha Starehe na cha Biashara

Balisidya, (1982) anatuambia kwamba, ukandamizaji wa wanawake unategemea sana mahusiano na dhamira ya kimapenzi, na akazibainisha dhamira tatu katika mahusiano yao: Uhusika wa mwanamke katika kuzaa na kulea watoto, uhusika wa kumstarehesha na kumfurahisha mwanamume na uhusika wa mwanamke kama mzalishamali. Kwa kupitia dhamira hizi tatu tunaona kwamba, mwanamke anahusishwa na kumstarehesha mwanamume ambapo, uhusika huu unagubikwa na elementi za ngono na kiuchumi. Kwa kuyathibitisha haya, Zainab Lipangile katika wimbo *Mama Afrika* anatukumbusha kuwa, uhusika huu unasababisha wasichana wadogo kufanya starehe na wazee, wanawake kuwastarehesha wavulana wadogo na hata wasichana wa shule kufanya ngono na wavulana wa mitaani. Msanii anawaasa wasichana kujishughulisha zaidi na masuala ya elimu na kuwaheshimu wazazi, ambapo ndivyo vitu vya msingi kwa mwanamke, vyenye kumwezesha kujikwamua kutoka kwenye makucha ya mwanamume dhalimu.

(3c) *... za kwa tunadhalilishwa na kuonekana, chombo cha starehe,*
*tujaribu kujitunza,*
*.... watoto wadogo, tusipende kutembea na wazee,*

*fuateni wosia hiyo tabia, isiendelee, tuzingatie elimu,*
*wazazi tuwape heshima watoto watia wazimu ...*

Msanii Barnaba ameielezea tabia ya mwanamke kutumika kumstarehesha mwanamume katika wimbo *Nabembelezwa* kwa kutuonesha jinsi mwanamke anavyofurahia maisha ya kubembelezwa, kudekezwa na mwanamume. Tazama maneno asemayo msanii huyu:

(4) ... *Nikilia nabembelezwa kwa upendo,*
*naye akinuna namliwaza kwa vitendo.*
*Je, wewe ushawahi kubembelezwa,*
*mwenzio mimi nishawahi kubembelezwa*
*Nadekezwa ah ah nabembelezwaa ah ...*

*..Mapenzi si mchezo naamin, wapendanao mapcha...*
*Nikilia nabembelezwa kwa upendo,*
*naye akinuna namliwaza kwa vitendo*
*Je wewe ushawahi kubembelezwa,*
*mwenzio mimi nishawahi kubembelezwa*
*Nadekezwa ah ah nabembelezwaa ah ...*

Katika wimbo huu, msanii amemchora mwanamke anayedhani kuwa, anapobembelezwa, anapodekezwa na kustareheshwa na mwanamume na hivyo lazima apate pia ujira wa kazi hiyo anayoifanya. Msanii anasema kuwa anajidanganya mwenyewe kwani ujira wake huo ni lazima uambatane na kufanya ngono na kupata malipo ya biashara ya ngono kujiingizia kipato. Uhusika wa wanawake hawa umejikita katika fikra kwamba, daima anayefaidika katika starehe hiyo ni mwanamume hivyo anastahili kuilipia. Hata hivyo, tukiangalia kwa undani uhusika huu wa kufanya ngono huzishirikisha na kuzifurahisha jinsi za kike na kiume. Kwa ushirikiano huo, tungeliunga mkono endapo jinsi zote zingelishirikiana kulipia starehe hiyo gharama. Hapa panazuka suala la kujidunisha kwa jinsi za kike kuwa mwanamume ndiye mwenye kumlipa mwanamke pesa kwa tendo walilolifanya pamoja. Suala hili la biashara ya ngono limemulikwa na msanii Twenty Percent (20%) katika wimbo wake *Yanini Malumbano*. Msanii anaonesha kuchoshwa na mwanamke huyu katika aya ifuatayo:

(5) *... Yanini Malumbano, ya nini Maneno,*
*Najiweka Pembeni naepusha Msongamano ...*
*Umalaya kasi kashika, Anagawa kwa Kila rika ...*
*Hebu shika talaka yako nenda nendaa, ...*
*Hata kama zamani nilipenda...*

Katika wimbo huu, msanii anaonesha jinsi baadhi ya wanawake wasivyothamini mapenzi ya dhati na hivyo kuamua kufanya biashara ya ngono na kila mwanamume anayejipitisha mbele yake. Msanii anamhusisha mwanamke huyu na msambazaji wa magonjwa ya ngono kama kisonono, kaswende na hata UKIMWI na hatimaye

anapewa talaka yake. Hata hivyo, pamoja na kwamba suala hili lipo nje ya mada yetu, tunaweza kutaja tu kwamba, dhuluma hii ndiyo inayopingwa na nadharia ya ufeministi kwani, inawafanya wanawake kudharauliwa na jamii kuwa wanaofanya biashara ya umalaya.

Masanii Dayna katika wimbo *Mafungu ya Nyanya*, anashadidia uhusika tulioutaja wa mwanamke wa kuvuka mipaka na kujiuza kwa bei rahisi kama yauzwavyo mafungu ya nyanya. Kwa kupitia msimbo wa mafungu ya nyanya yanavyochaguliwa na wanunuzi ndivyo makahaba wanavyojipatia mahitaji yao. Tutafakarini maneno ya wimbo yafuatayo:

(6) *... Mnatugeuza mafungu ya nyanya,*
*Na kisha mnauza??,*
*Mkifunua mnafunika,*
*Inaniumiza mtima ...*

Msanii Dayna anatumia msimbo wa mafungu ya nyanya kuwasema wanawake ambao kila kunapopambazuka hujipanga barabarani wakisubiri wateja wa kuwachukua. Anaonesha kuwa, wanunuzi wanapowasogelea, wanawake hawa hutumia kila mbinu ili waweze kumvutia mlengwa. Kwa kutumia msimbo wa mafungu ya nyanya, Daina anaionya jamii kujiepusha na biashara haramu ya ukahaba ambayo mwisho wake ni mbaya.

### 4.3 Mwanamke Kunyimwa Fursa za Elimu na Siasa

Takwimu za mtandao wa jinsia (TGNP 2001) zinabainisha kwamba, 25% ya wasichana huacha shule kabla ya kumaliza masomo yao kwa sababu za kuolewa, mimba, utoro, uchumi duni, mazingira mabaya ya kielimu, mila potufu nakadhalika. Buchert (1994) anadai kuwa, mila na desturi za jamii za Kiafrika zinahimiza kuwa, kazi za mwanamke katika jamii zinatofautiana na zile za mwanamume, kutokana na kiwango cha elimu wanachokuwanacho. Buchchert (khj) anasema kuwa, mwanamke anafundishwa namna ya kuwa mlezi bora wa familia, kulea watoto, kumtunza mume ilhali mwanamume hufundishwa kuwa mume mzuri na kiongozi wa familia. Suala la wanawake na elimu limesawiriwa na msanii Vick Kamata katika wimbo wake wa *Wanawake na Maendeleo*. Katika wimbo wake huo, msanii anawahimiza wanawake kujituma katika kazi ili waweze kujiendeleza na kuziendeleza familia zao.

(7) *... Ni nani kama mama, jamani nauliza,*
*Walimwengu naomba nidhirishieni,*
*nafikiria hakuna aliye kama mama,*
*na tena hathaminiwi, hapewi haki yake.*
*... Tangu enzi za mababu, yaeleweka wazi,*
*mama ndiye mlezi hakuna jamii, amka mwanamke...*
*jamani ofisini mwanamke chapakazi,*
*Mloko bungeni teteeni, haki zetu tuhimize.*

*mabinti wapende shule ili wasijenge jazwa kwa kukosa elimu............*

Vick anawaamsha wanawake kutoka usingizini na kujibidiisha katika kufanya kazi hususani wale wanaokaa wakisubiri kuletewa kila kitu na wanaume. Anadai kwamba, wakati wa sasa ni wa kuzalisha mali kwa pamoja ili kuwapa watoto haki zao za msingi yaani, elimu bora. Msanii anawashauri wanawake kutambua kuwa, elimu inatakiwa imkomboe mwanamke kutokana na mfumo kandamizi na unyanyaswaji unaofanywa na mwanamume. Anawakumbusha wanawake kuwa elimu itazisaidia jamii kuondokana na mawazo na mila potofu zinazowapangia wanawake nafasi ya kumstarehesha, kumtumikia na kumtii mwanamume kwamba, ndiyo stahiki yao. Msanii anahitimisha akisema, elimu itawawezesha wanajamii kujenga mawazo ya kujadili na kumfanya mwanamke aondokane na unyonge unaosababishwa na utamaduni unaobebwa na mila potofu.

Kimsingi elimu ina mwelekeo wa kuongeza fursa sawa ya wanawake kupata ajira na ushirika wao katika siasa na maamuzi. Ndio sababu msanii Nakaya Sumari katika wimbo wa *Mr Politician* akasema:

(8) ... *Miaka ya juzijuzi uliomba kura zetu,*
*Ahadi nazo ulizimimina Elimu bora,*
*Afya bora, barabara nzuri, Ajira nje nje,*
*Leo sioni mabadiliko hali imekuwa ngumu,*
*Eti wajiita Mr. Politician ...*

Nakaya amewakumbusha wanawake kuwa, hawashirikishwi katika maamuzi ya kisiasa na yale yanayohusu uongozi ambapo, hata wakishirikishwa, wengine huonekana wakitoa ahadi za uongo kwa manufaa ya vyama wanavyoviwakilisha. Anadai kuwa, wanawake hawana mwamko katika masuala ya kisheria, yanayowapelekea kutokujua haki na majukumu yao. Kimsingi, elimu wanayoipata wanawake inalenga katika kuongeza fursa sawa ya kupata ajira na ushirikishwaji katika maamuzi pamoja na wanaume. Kwa kupitia elimu wanawake wanaweza kupanga vizuri maisha yao, kufanya maamuzi ya kutekeleza shughuli zao za kawaida kama uzazi wa mpango, kushiriki katika shughuli za kisiasa na matumizi bora ya raslimali zilizomo katika jamii.

## 4.4 Mwanamke kama Kiumbe Tegemezi

Momanyi, (2000) na Mbilinyi na wenzake, (1991), wamemwonesha mwanamke alivyochorwa kama kiumbe kinachomtegemea mwanamume wakati wa taabu au matatizo. Wanawake wanawategemea wanaume wanapofilisika, wanapokosa fedha, mahitaji yao muhimu na kadhalika. Utegemezi wa mwanamke kwa mujibu wa nadharia ya ufeministi umejitokeza pale mwanamke anapotafuta ushauri, msaada, hifadhi na hata huduma. Wanaume katika jamii nyingi za Kiafrika wamepewa nafasi ya juu ya kumiliki njia kuu za uchumi, hivyo kuwa na maamuzi ya mwisho juu ya

majaliwa ya wanawake. Tunamaanisha kuwa, wanaume ndio wanaotoa maamuzi juu ya mwanamke kukaa ndani au kufanya shughuli ya kuzalisha mali katika jamii. Mazingira haya yaliyotengenezwa na wanajamii juu ya mwanamke yamemfanya mwanamke amtegemee mwanamume katika shughuli zote ndani ya familia inayomzunguka. Hata mwanamume anapokuwa mbali na nyumbani, mwanamke mtegemezi huhitaji kuongozwa na mwanamume. Msanii Diamond Platnum anausawiri ukweli huu katika maneno ya wimbo *Nitarejea*:

(9) *...Huwa nakosa raha, kweli nikikosa cha kutafuna,*
*Roho yangu inauma, sema ntafanya nini na pesa sina. …*
*maneno yako yanafanya, nakosa raha na mawazo …*
*...Unapokwenda kama ukifika salama,*
*utukumbuke na sisi usisahau kama mkeo na wana,*
*umetuacha na dhiki…*

Msanii Diamond anatuonesha baba wa familia akiagana na familia yake ambapo mwanamke anaonekana kumlilia yeye na nafsi yake na ya jamii inayomzunguka kuwa atakuwa mgeni wa nani pale kijijini. Neno *nitarejea*, linatutanabahisha kuwa, mwanamume kawaida ni mtu wa kutafuta mali na mwanamke humtegemea mwanamume kwa kila hali. Kwa upande mwingine, mwanamke akitumiwa na Diamond kama mshauri wa mwanamume. Tunamwona mwanamume akimshauri mke wake akisema:

(9b) *…..Vile usijali, na naomba chunga sana,*
*ogopa marafiki, wakikulaghai hata kwa mbegu za mtama,*
*waambie sidanganyiki…..*

Mara nyingine utegemezi huo hufikia mwisho, pale mwanamke anapojigundua kuwa na uwezo mkubwa kifikra na kiuchumi na hivyo, kugundua haki aliyonayo juu ya mwanamume. Kutenguka kwa utegemezi huo kunamletea mwanamke heshima, mamlaka na uwezo wa kuiongoza familia na jamii. Tunayo mifano mingi inayodhihirisha kuwa, wapo wanawake wenye madaraka na heshima kuwazidi wanaume na ambapo hawawategemei wanaume si kwa hali na wala kwa mali. Tunawashauri watafiti, wasanii na watunzi wa nyimbo za kizazi kipya kuzichambua kazi za sanaa kwa kuzingatia vigezo vyote vinavyosadifu hali halisi ya uhusika wa mwanamke katika jamii na kuacha kuwadanganya wasomaji wa kazi zao kuhusiana na usawiri usiohalali wa mwanamke. Wasanii waioneshe jamii kile kilicho na ukweli kuhusiana na mwanamke kwa sababu, dunia ya jana imepitwa na wakati.

### 4.5 Mwanamke kama Kiumbe Mwenye Mapenzi na Mshawishi

Katika jamii zetu nyingi, mwanamke anaonekana kuwa ndiye chanzo cha matatizo ya kimapenzi, kiuchochezi na kiushawishi. Suala la mapenzi, limemfanya mwanamke kuonekana malaya, mshawishi, msaliti na mbabe. Mwanamke anaoneshwa kumsaliti mumewe kimapenzi punde mumewe anapoonekana kutokuwa na kipato cha kuihudumia familia yake, na hivyo kumfanya mkewe kujihusisha na

kutafuta fedha za kuitunza familia kutoka kwa wanaume wengine. Senkoro, (1982) anatuonesha uhusika huu kuwa, mwanamke anachorwa, anabainishwa na kusawiriwa katika taswira hiyo kutokana na kiu waliyo nayo wanaume. Utafiti wetu umeshuhudia jinsi baadhi ya wasanii walivyoichambua tabia hili ya wanawake kudharauliwa na kushushiwa hadhi na kunyanyaswa hivyo. Dharau na manyanyaso ya wanaume kwa wanawake yaliangaliwa na msanii Judith Wambura, yaani Lady Jay Dee katika wimbo wake *Wanaume Kama Mabinti*. Sehemu ya wimbo huo ni hii ifuatayo:

(10) *... Mnakula, kunywa na kuvaa, siku zinaenda,*
*Vya bure hupenda kupewa wala hamna fikira.*
*Kila upande wanafiki, Siku zinaenda,*
*Vinywa vimejaa ufitini, Wanaume kama mabinti...*
*... Ninaposema wanaume simaanishi wote,*
*Ila wale wenye tabia, kama za mabinti,*
*Utawaona kwenye magari ya 'mademu' zao ....*
*Tuwatofautisheje na machangudoa ...*

Katika wimbo huu, msanii anawasema wanawake wenye kugawa mapenzi kwa kufurahia maisha ya kifahari ilhali wanachodanganyiwa ni kwa ajili ya mapenzi au ngono tu. Mara nyingi wanawake wengine huonekana wakiwashawishi wanaume kwa mienendo yao ambayo kwa namna moja au nyingine hushawishi matendo ya dhuluma, ukatili na udanganyifu kwao. Hali hii imekuwa ni ya kawaida kabisa kwa wanawake kudanganywa kwa maneno matamu kama vile *nitakuoa*, *nitakujengea nyumba*, *nitakununulia gari zuri* au hata *nitakusomesha*, na matokeo yake ni kukwama kwa wanawake waliokuwa wengi kimaisha. Wanawake hawa wamekuwa wakiwaamini wanaume kiasi cha kukubali hata kufanya nao ngono na nyingine zikiwa ngono zembe zilizosababisha kupatikana kwa mimba za utotoni na zisizotarajiwa, magonjwa hatarishi na yasiyotibika na madhara mengine mengi.

Endapo mchambuzi atausikiliza wimbo huu wa Lady Jay Dee kwa masikio ya kihakiki, atagundua kwamba, kwa upande mmoja, unawadhalilisha wanaume, wanaowategemea wanawake wenye uwezo na mali kupata huduma na mahitaji yao ya kila siku. Wanaume kama hawa ni wengi na kwa siku kama hizi sasa wamejipatia umaarufu mkubwa sana wa kutumiwa kutoa huduma ya mapenzi kwa wanawake wenye pesa, magari na maisha ya anasa huku wakipata malipo ya fedha na mali nyingi kutoka kwa wanawake hawa. Kwa upande wa pili, Lady Jay Dee kwa kupitia maneno ya wimbo wake huu anajidhalilisha yeye mwenyewe pamoja na wanawake wengine wengi wanaodhani kwamba, wao ndio wanaostahili kupewa ofa, kuhongwa na hata kupewa zawadi na wanaume. Lady Jay Dee anaonekana kulemazwa kiakili na kifikra na mfumo dume uliouathiri kwa kiasi kikubwa uimbaji wake na uliosababisha kuwasema vibaya mabinti kwamba, ndio wenye haki ya kupenda kupewa vya bure na wanaume.

Kadhalika, wapo wanawake wengine ambao hufurahia kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanaume, lakini moyoni mwao hawana mapenzi ya dhati. Mawazo ya wanawake hawa huwa yanajikita kwenye starehe, kujirusha viwanjani na "kuwachuna" wanaume. Wanawake hawa wasiokuwa na mapenzi ya dhati hudiriki hata kutoa rushwa ya mapenzi kwa wakuu wa dini ili waweze kuwasaidia kutatua matatizo yao ya asasi ya ndoa. Haya ameyaona msanii Janguar na kuyaonesha katika wimbo wake wa *Kigeugeu*. Katika wimbo huo, ameonesha namna wanawake walivyo vigeugeu katika ndoa zao. Wanawake hawa hawathamini nafasi zao katika ndoa na ndio sababu ya wao kujikuta wakifanya kinyume na taratibu za ndoa. Msanii anatumia wimbo huu kuifunza jamii ibadilike na kutii ndoa zao na zile za watu wengine, na pia kujali nafasi zao katika jamii inayowazunguka. Msanii anatueleza:

(11) *... Nimuamini nani nimwache nani,*
*Mana kila ninayemwamini mwishowe, Ananigeukia,*
*nikimwacha Mchungaji anaingia ndani,*
*Kuzini na Mke wangu...*

Wapo wanawake wengine ambao hupenda kutumia maumbile ya miili yao kuwashawishi wanaume ili waweze kuzivuruga mapenzi ya ndoa zao. Wanawake hawa huwashawishi wanaume kwa kuomba urafiki wa kawaida tu, kisha wanapozoeana urafiki ule hubadilika na kuwa mapenzi ya kweli. Mapenzi haya yamwingiapo mwanamume humbadilisha na kumdharau au kumwacha kabisa mwanamke wake wa ndoa. Mapenzi haya ya kiushawishi yanayoendeshwa na mwanamke (aliyemteka mume wa mtu) humalizikia pabaya, yaani dhambi ya kuipatia majibu yake kiama na kusambaratisha jamii (mke na watoto) kwa mapenzi ya kiushawishi. Haya yanaoneshwa katika wimbo wa Ally Kiba ***Mapenzi Yana-run Dunia***, kwa kupitia maneno yafuatayo:

(12) *... mwenzio mimi ni mtulivu na kuiba mali ya mtu sijafunzwa,*
*Unadhani kama uliyonipa mimi leo inaniuma,*
*Fikira zako ziko vibaya kwa kudhani ya kwamba yule demu nilimpenda,*
*Ni kweli nilimpenda lakini ni kama rafiki wa mtima.*
*Haya uliyofanya leo ikifika kesho utajibu nini kiama.*
*Kwa yote mapendo ni kama kioo aliyokupa niliyaona na mimi nakusaliti*
*... Unatema bigijii, kwa karanga za kuonjeshwa,*
*najua mwanamke akipenda kapenda kweli mimi na run dunia...*

Kupitia maneno ya wimbo wa Ally Kiba *Mapenzi Yana-run Dunia*, tunaoneshwa jinsi mwanamke anavyoweza kutumia uhusika wake wa ushawishi kuvuruga asasi za ndoa ya mapenzi, kusambaratisha wapendanao, kuchochea migogoro na kugombanisha wapendanao. Wanawake wamekuwa vishawishi kwa wanaume kwa mienendo yao ya kutembea nusu uchi. Wanawake wamekuwa waking'ang'ania wanaume hususani wenye ndoa kiasi cha kufanikiwa kuwanasa katika mitego yao ya

kishawishi. Aidha, tunashauriwa kwamba, mtu mwenye mume na mwenye mke (aliyeoa au kuolewa) anatakiwa ajiheshimu mbele ya jamii inayomzunguka.

**4.6 Mwanamke kama Kiumbe Laghai aliyenyimwa Mapenzi**

Mwanamke amesawiriwa kama kiumbe kisichokuwa na mapenzi ya kweli kwenye nyimbo za kizazi kipya tulizoziona hapo awali, akihusishwa na biashara ya ukahaba. Tunamwona msanii 20% katika wimbo *Ningekusamehe* baada ya kuchoshwa na mwanamke aliyempenda na aliyemuoa akawa anaishi naye. Baada ya kijana huyu kupata kazi Ulaya, aliamua kumwacha mke wake huyu nyumbani kwake na kwenda kutafuta fedha za kuitunza familia yake. Baada ya muda aliamua kurejea nyumbani akamkuta mkewe amechukuliwa na mwanamume mwingine. Alihangaika kumtafuta, kumbembeleza ili warudiane, kisha baada ya muda yule mwamanke akaamua kurudi kuomba msamaha. Ndipo sehemu ya wimbo huo ikaendelea hivi:

(13) *... Naomba ondoka inge mwenye mapenzi ya kweli asije akakukuta,*
*Ningekuwa nawe ila wewe unapenda sana pesa,…*
*Ningekusamehe ila tayari nimekwisha mpata mwingine, ...*
*Ni nani aliyetaka kunitoa roho penzi likafika mwisho...*
*Sina habari, sitaki kuwa nawe, tena huna nafasi ndo hivyo nishakutema,*
*Nakupa fact, unielewe kiundani sina mapenzi kwako*
*yalikuwepo tangu zamani, ... nenda tu niache...*

Kwa kupitia wimbo *Ningekusamehe* tunauona uhusika huu wa mwanamke ulivyoathirika mara inapogundulika kuwa mwanamke hana mapenzi ya kweli kama ilivyotegemewa na mume wake. Hii ni tabia ya kupenda mtu kwa tamaa ya pesa, ambapo yanaibuka maswali ambayo yanahitaji maelezo ya kina kuwa: Je, ni kwa nini mwanamke ajiingize kwenye mapenzi ya pesa baada ya mume kusafiri kutafuta pesa? Je, pesa ndicho kipimo cha ndoa kwa mwanamke?

Kwa upande mwingine, tunamwona mwanamke akiutumia uhusika wake kumlaghai na kumghilibu mwanamume kwa maneno matamu ya *nisamehe*. Haya tunayasikia yakiwa yameibeba sehemu ya usuli wa wimbo *Ningekusamehe*, ambapo mwanamke anasema:

(14) *…Mimi yakale achana nayo, Niko chini ya miguu yako,*
*Basi mpenzi, mbona wanipa kazi, bila wewe siwezi nitajawa na simanzi,*
*mwenyewe wajua jinsi gani nimekufia, Basi nakwimbia usiweze kunikimbia,*
*unajua sina ujanja wa kuachana nawe, kuniacha njiapanda, nitapata kiwewe,*
*huyo mtimue mi unirudie, usiniache nilie, wewe ni wangu mie, ……….*

Hapa tunaoneshwa aina mbili za mapenzi yanayomsibu mwanamke, yaani mapenzi ya dhati na mapenzi ya ulaghai ambayo ni ya uongo. Mwanamke wa pili mwenye mapenzi ya dhati anampenda mume wake kwa dhati, ilhali yule wa kwanza ameonekana akichanganya wanaume kwa tamaa ya fedha. Aidha, kwa upande wa

uhalisia, mwanamke hushawishika kutumia ulaghai ili aweze kujinasua kutokana na ugumu wa maisha unaomkabili mwanamke huyu na hata jamii nzima kwa ujumla.

**4.7 Mwanamke Kama Mzazi, Mlezi, Mwenye Mapenzi na Huruma**

Mwanamke amehusishwa na uzazi, ulezi, upendo na huruma; yaani mtu anayekubalika katika jamii. Aidha, mwanamke ameoneshwa akiwa mtu mwenye mapenzi, mkarimu na kiongozi, ambaye daima huiongoza jamii katika kuuona mwanga bora na kuyaongoza maisha yao. Uhusika wa mwanamke huyu unachorwa hivi na wasanii wenye kuheshimu maongozi, maoni, maonyo na maelekezo yatolewayo na yaendeleayo kutolewa na wahusika hawa katika jamii zetu. Uhusika wa aina hii umeonwa na baadhi ya wasanii wa kizazi kipya kama Banana Zoro na wimbo wake *Mama Yangu*, usemao:

(15) *... Mama yangu, wewe ni nguzo maishani mwangu,*
*Taa imulikayo mbele yangudaima milele…*
*Mawazo yako mama yanaongoza maisha yangu,*
*Ni tuzo gani unayostahili, wa kuweza kuthamini,*
*shida zangu usumbufu wangu toka kuzaliwa kwangu, na mpaka leo,*
*nasimama mbele yako mama,*
*unastahili sifa kwa mapenzi uloonesha kwangu tngu nazaliwa………*
*Na hukuchoshwa na wangu usumbufu,*
*muda wako mwingi ulitumia kwa ajili yangu ….*
*Nakumbuka mambo uliyoniruhusu na kunikataza, mazuri ulonifanyia,*
*Nashindwa kushukuru ...*

Katika wimbo huo, msanii ameshindwa kuficha mambo yote mazuri yanayofanywa na wanawake, na pia ameshindwa la kusema anapoiona jamii ikimshushia hadhi, inamdhalilisha na kumhadaa mwanamke. Banana Zoro amehusisha umuhimu wa mama mzazi na mlezi na nguzo ya familia kwa sababu, msingi mkuu wa maendeleo ya mtoto huanza kujengwa na mama. Mama pamoja na kuwekwa katika nafasi ya chini na mfumo dume wa kijamii, msanii amemchora kama ndiye aliyeshikilia nafasi ya juu katika malezi na makuzi ya jamii. Mama anachambuliwa kama taa yenye kutoa mwangaza wa kumwongoza mwanajamii katika maisha yake, ndio maana mawazo ya mama aliyoyapitishia kwa mtoto humwongoza na kumwelekeza maishani mwake.

Katika kujadili uhusika huu wa mwanamke, tunaona kuwa masuala ya huruma, upendo na uvumilivu yamejengwa katika msingi wa kimaumbile tu. Mwanamke amejaliwa kuwa na huruma nyingi ingawa kuna kipindi huruma hizo hudharauliwa. Kwa mfano, pindi itokeapo mtoto wake wa kike kukosa uzazi, basi anayetuhumiwa kusababisha hali hiyo mara nyingi huwa ni mama yake mzazi. Hayo na mengine mengi huvumiliwa na mwanamke kwa kuwa, kwa asili ya maumbile na kibiolojia mwanamke ni mtu mwenye huruma, upendo na uvumilivu kwa kiasi kikubwa.

### 5.0 Changamoto na Mapendekezo

Uhusika wa mwanamke katika jamii zetu bado ni suala lenye kuhitaji mijadala ya ziada katika ulimwengu huu wa utandawazi, ukweli na uwazi. Nchini Tanzania, bado mwanamke anadhalilishwa, kubaguliwa na kupewa uhusika duni wenye manyanyaso na baadhi ya wanajamii. Kumekuwapo na kubaguliwa kwa mwanamke katika nyanja za elimu, siasa, kijamii, michezo, na kadhalika kila wakati pasipo kujali usawa wa kijinsia. Kwa upande wa utamaduni, mila, desturi na dini, mfumo dume bado ungali unashikilia mpini ilhali mfume jike ukiwa umeshikilia makali. Tunajiuliza, ni kwa nini mwanamke anawekwa katika daraja dhaifu na ni kwa muda gani ataendelea kusawiriwa namna hiyo? Je, mwanamke afanye nini katika kujinasua kutoka katika wimbi hili lililomsibu kwa kusawiriwa na wasanii? Sehemu hii ya mwisho wa makala yetu inajaribu kutoa majibu kwa maswali haya, na pia kuzitaja changamoto zilizopitiwa katika kuandika makala haya kama ifuatavyo:

Mosi, uchunguzi tulioufanya umedhihirisha kwamba, wanawake wamedhalilishwa sana na baadhi ya wasanii wa nyimbo za Kiswahili kiasi cha kuyaathiri maendeleo yao katika jamii. Katika makala yetu, tunajiuliza: Je, mwanamke anazo haki gani katika jamii yake kwa mujibu wa sheria za ndoa za kijadi? Je, mwanamke anao usalama gani anapolazimishwa kuishi na mwanamume asiyemjali, la sivyo atanyang'anywa watoto? Je, ni kwa nini wanaume waruhusiwe kuwatalakisha wanawake ilhali wanawake wakanyimwa mamlaka hayo? Majibu ya maswali haya ndiyo suluhisho la makala yetu.

Pili, Balisidya, (1982) anasema kuwa, mwanamke kufananishwa na chombo cha kumstarehesha mwanamume ni suala linalohitaji mjadala mrefu. Tunakubaliana naye kwamba suala hili linahitaji kujadiliwa kwa undani zaidi kwani ni dhana potofu, isiyokuwa na mashiko. Wasanii wetu wanashauriwa wayadhihirishe maneno yao kwa vitendo na sio kuimba tu majukwaani.

Tatu, masuala ya kumtumikisha mwanamke kama mzalishaji mali mkuu, kulea familia, kupika, na kadhalika ni matendo yasiyostahili kufumbiwa macho katika fasihi ya Kiswahili. Mwanamke anastahili kuheshimiwa, kupewa haki ya kushiriki na kufanya shughuli zote anazoshiriki na kuzifanya mwanamume.

Nne, mgawanyo wa majukumu kati ya mwanamke na mwanamume ni chanzo kimojawapo cha unyanyaswaji wa wanawake katika jamii zetu. Suala hili linatakiwa lifanyiwe kazi kwa sababu, mila na desturi za jamii nyingi zinauhalalisha ukandamizaji wa wanawake.

Tano, Mwanamke apewe elimu na kujengewa uwezo wa kujiamini kuwa anaweza kumwongoza, kumtawala na kumwelekeza mwanamume.

Makala inapendekeza mambo kadhaa yafanyike ili kuuepusha uhusika wa udhalilishaji, ukandamizwaji na udunishwaji wa mwanamke katika jamii zetu kupitia nyimbo za kizazi kipya kama ifuatavyo:

Mosi, makala inaitambua nafasi waliyopewa wanawake ndani na nje ya jamii zetu, ambapo wanaume walio wengi hutumia muda mwingi wakiwa mbali na nyumbani kutokana na shughuli za kiuchumi na zile tunazoziita za kijamii. Watoto kwa kiasi kikubwa huathiriwa zaidi na malezi ya mama na hivyo, kumfanya mwanamke kuhusika pakubwa na malezi na kuiendeleza jamii.

Pili, makala inapendekeza kwamba, elimu iwe mkombozi kwa mwanamke, imkomboe kutoka katika mfumo dume, ukandamizaji, udhalilishaji na ubaguzi unaozizunguka jamii zetu. Pia, elimu itaisaidia jamii kuondokana na mawazo, mila na desturi potofu za kusema kuwa nafasi aliyopewa mwanamke ni mapenzi ya Mungu na ndiyo stahiki yake. Elimu itaiwezesha jamii kujenga mawazo na kutoa fursa sawa kwa jamii nzima kumjadili na kumnasua mwanamke aondokane na unyonge aliokuwa nao dhidi ya mwanamume.

Tatu, makala inawashauri wasomi na wasanii chipukizi watumie nafasi zao katika kuusawiri, kuutangaza na kuupigania uhusika chanya wa mwanamke katika kazi zao. Wasanii waoneshe uhusika wa mwanamke unaozingatia usawa wa kijinsia, usiosawiri ubabe au usambazwaji wa mfumo dume dhidi ya mfumo jike.

Nne, makala inawahimiza wasanii wa nyimbo za Kiswahili kuuchora uhusika wa mwanamume sawa na wa mwanamke. Kwa kufanya hivyo, jamii itaelewa na kuelimika kuwa, tabia hizo kwa namna tofauti, zinanuia kuwachafua wanawake wa jamii husika.

## 6.0. Hitimisho

Tumeona kwamba, mwanamke amedhalilishwa, amekandamizwa na kuonewa kupitia nyimbo za Kiswahili, zilizomchora mwanamke katika taswira za uzinifu, ubidhaishwaji, chombo cha kumstarehesha mwanamume na kuzalishia mali. Wanawake wameoneshwa kutokuwa na umuhimu mwingine katika jamii, mbali na kuwalea watoto na kuwatumikia wanaume. Baadhi ya nyimbo zimewahusisha wanaume kama wasimamizi wakuu wa majukumu na mali za familia na jamii.

Baadhi ya wasanii, kupitia nyimbo zao wameyaonesha mambo kadha wa kadha yanayoufikisha ujumbe chanya wa kuzielimisha na kuziokoa jamii zetu. Ni kwa kupitia wasanii wetu hawa, wanaume na wanawake wanaweza kushawishiwa kupambana na mfumo dume unaomnyanyasa mwanamke hadi mafanikio yapatikane.

Muhando, (1982) ameeleza waziwazi kuwa, juhudi za kumkomboa mwanamke zitapatikana tu pale wanawake watakapoungana na kushirikiana katika kupambana na dhuluma. Hivyo, pamoja na kushirikisha wanaume, mwanamke ndiye mwenye uwezo wa kukataa unyanyaswaji na kupambana katika kujikwamua katika hali hiyo na sio kungojea kukwamuliwa na mwanamume.

La tamati, wakati wa mfumo wa siasa ya ujamaa na kujitegemea kulikuwa na asasi za kiraia (NGOs), chache sana, ambazo zilikuwa na uwezo duni wa kudai usawa katika uhusika wa mwanamke na mwanamume. Vyama mbalimbali kama Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Umoja wa wazazi (TAPA), na vingine havikuwa na nguvu ya kutosha katika kuleta mabadiliko ya kweli ya kijinsia, kwani mfumo dume ulikuwa umeshamiri. Uhuru wa vyombo vya habari wa kutangaza na kueneza sera ya usawa wa mwanamke na mwanamume ulikuwa duni mno. Hivi sasa jamii za Kitanzania, zimezingirwa na mfumo wa soko huria, utandawazi na teknolojia mpya unaowawezesha wanawake wa Kitanzania kuona jinsi wanawake wenzao ulimwenguni wanavyopambana kudai haki, na baadhi yao kufaidi haki na usawa kati yao na mwanaume. Mazingira haya tuliyo nayo yanatoa fursa nzuri zaidi kwa wanawake kuweza kufanikiwa katika harakati zao dhidi ya kunyanyaswa, kunyimwa haki, kutumiwa kama vyombo vya starehe na vya kuzalishia mali, kumtumikia mwanamume, na kugeuzwa vyombo vya kuzaa na kulea watoto.

## Marejeo

Balisidya, M.L. (1982). *The Image of the Women in Tanzania Oral Literature*. Dar es Salaam: *Kiswahili* Juzuu Na. 49/2, TUKI.

Biblia, (1989). *Kitabu cha Mwanzo (2:21 – 22).* United Bible Societies.

Guethel, A. (1981). *Sociology of Housework,* New York, Pantheon Books.

Khonje, M. (1979). *Some Notes on the Rule of Women on Maintainance of Women Oppression by Men*. Dar es Salaam: BRAULUP.

Koda, B. (2000). *The Gender Dimension of Land Rights in Tanzania: Case Study of Msindo Village, Same District*, Unpublished Ph.D Thesis, UDSM.

Lughano, R (1989), "Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi", Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Lyatuu J. (2011) *Usawiri wa Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Waandishi wa Kike na wa Kiume katika Riwaya Teule.* Haijachapishwa Tasnifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mackinnon, C.A. (1991). *Toward A Feminist Theory of the State*. London, Havard University Press.

Mazrui A. (1982). *Kilio cha Haki*. Nairobi: Longman.

Mbilinyi, M. na Wenzake (1991). *Wanawake Tanzania*. Uchambuzi wa Harakati zao za Ukombozi. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Momanyi, C. (2002). *Suala la Uana katika Utafiti wa Fasihi ya Kiswahili*. Katika Utafiti wa Kiswahili - Makala za Kongamano la Chama cha Kiswahili cha Taifa – Kenya 2002. Katika. Nairobi: Moi University Press.

Morris, P. (1993) *Literature and Feminism.* Oxford Black.

Muhando, P. (1982). *Nguzo Mama*. Dar es Salaam: University Press, Dar es Salaam.

Mwachofi, A.K. (1987). *Mama Ee*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Ndung'o, C. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. University Press

Ngaiza, M.K. (2002). *Gender Dynamics in Poverty Alleviation in Tanzania: Ngara District Case Study*, Unpublished, Ph.D. Thesis, UDSM.

Omari, S. 2009. *Mtindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya.* katika *Kiswahili*: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Juzuu 49/2, (mh) Massamba D. P. B., Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TGNP, (2001). *Kuelekea kwenye Usawa:* taswira ya mwanamke Tanzania. Dar es Salaam. SARDC.

Senkoro, F.E.M.K. (1982). *The Prostitute in African Literature*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Shayo, R. (2004). *Towards Promoting Gender Equality and Equity in Higher Learning Institution: The Case of the University of Dar es Salaam, Tanzania,* in: Tanzania Journal of Development Studies, Vol. 5 No. 3, Pp 53-74.

Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi*. *Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi, Phoenix Publishers.

**Discografia**

Ally Kiba, ( 2012). *Mapenzi Yana-run Dunia*. Dar es Salaam: Royal Production.

Banana Zoro, (2002). *Mama Yangu*. Audiocassete. Dar es Salaam: FM Radio

Barnaba Boy, (2006). *Nabembelezwa*. Dar es Salaam: Sauti za Bongo Entertainment.

Ben Pol (2005). *Nitakupata.* Dar es Salaam: Umoja Audiovisual (EA) Ltd Vol. 17

Dayna Feat Marlaw, (2006). *Mafungu ya Nyanya*. Dar es Salaam: Emptysoulz Production, MJ Records

Diamond Platnamz, *Nitarejea*. Dar es Salaam: Bongo Flavour Audio CD, Vol. 3

Jaguar Kenya, *Kigeugeu.* Ogopa Video Presents: *www.ogopadeejays.co.ke*

Lady Jay Dee, *Wanaume kama Mabinti.* Dar es Salaam: Bongo Flavour Audio CD, Vol. 3

Mwasiti Ft. Linnah, *Nalivua Pendo.* Bongo Flavour Audio CD, Vol. 4

Nakaya Sumari (2010) *Mr Politician*. Dar es Salaam: Bongo Flavour Audio CD, Vol. 4

Twenty Percent, (2007). *Ya nini Malumbano.* Dar es Salaam: Royal Production.

Vick Kamata, (2005). *Wanawake na Maendeleo.* Dar es Salaam: Umoja Audiovisual (EA) Ltd Vol. 17

Zainab Lipangile, (2007). *Mama Africa*. Dar es Salaam: Royal Production.